

**KANUNI YA  
MWENENDO**

*Watu na Mazingira  
Hustawi Wakati...*



## CONTENTS

Ujumbe kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wetu juu ya Kanuni yetu ya Maadili // 2

Ujumbe kutoka kwa Afisa Mkuu wa Maadili, Ushirikiano na Faragha // 3

### Watu na Mazingira Hustawi Wakati...

Jitolea kwa Maadili Yetu // 4

Elewa Matarajio na Majukumu Yetu // 4

### Kuheshimiana

Jiendesha kwa Tabia ya Kitaalamu na kwa Heshima // 5

Kujitolea kwa Kutofautiana, Kutenda kwa Uhaki na Kunufaika Kutokana na Tofauti Zetu // 6

Kujishughulisha katika Mazungumzo Bora // 7

### Kuheshimu Ulimwengu

Heshimu Jamii Zote // 8

Kuheshimu Kuunga Mkono Uendelezaji wa Haki za Kibinadamu // 9

Kutenda kwa Uendeleu katika Kazi Yetu // 10

### Kutenda kwa Uadilifu

Fuata Sheria na Masharti yanayofaa na Kuepuka na Ulaghai, Wizi na Ufisadi // 11

Wanatenda kama Wasimamizi Wazuri wa Pesa Zote za Mchango na Mfadhili // 12

Kaa Salama na Ulinde Wengine // 13

Kuepuka na Migongano ya Maslahi // 14

### Kulinda TNC

Jitahadhari kwa Mitandao ya Kijamii na kauli za hadharani kuhusu TNC // 15

Hifadhi Hali Yetu ya Utoaji wa Misaada // 16

Weka Taarifa ya Siri Salama na Kueshima Faragha // 17

Linda Mali ya Kitaaluma // 18

Kulinda Rasilimali za TNC na Kutumia mifumo ya Taarifa kwa wajibu // 19

### Kujitolea Kwetu

Nini itafanyika nikifanya ripoti? // 20

Nini itatokea kama mtu analipiza kisasi dhidi ya mfanyakazi kwa sababu ametoa ripoti? // 20

# *Ujumbe kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wetu juu ya Kanuni yetu ya Maadili*

Kila siku tunaendelea kushuhudia mapambano ya sayari yetu dhidi ya mabadiliko ya hali ya hewa, na upotezaji wa biolojia- na kama matokeo, kuwekwa kwa mazingira yetu, na jamii zetu katika madhara. Tunaona pia jinsi vitendo vya ukosefu wa haki za kijamii, usawa, na vurugu vinavyochangia kwenye mapambano haya.

Tunapo pitia nyakati hizi ngumu, ni muhimu sana - sasa kuliko wakati mwingine wowote - kujiendesha kwa njia ambayo inashikilia maadili yetu na kuhakikisha kwamba tunawatendea watu wote kwa hadhi na heshima.

Tangu mwaka wa 1951, TNC imefanya kazi kwa pamoja na wanasayansi, jamii, mashirika ya hisani, na viongozi kutoka kwa serikali na tasnia, ili kulinda ardhi na maji ambayo maisha yote yanategemea.


Leo sisi ni shirika la kimataifa, na tuko na mtandao mpana na anuwai wa wafanyikazi, wenye hiari, na wafuasi kutoka duniani kote. Mtandao huu uliojitolea, una jukumu muhimu katika kusaidia TNC kufanikisha kazi yetu muhimu ya kulinda ardhi na maji ambayo maisha yote yanategemea.

Kuungana ni chombo chetu hodari ya kuunda maendeleo ya kudumu kwa sayari yetu - lakini lazima kwanza tujenge uaminifu, ili kufanya kazi vizuri kwa kila mmoja. Ni jukumu la TNC kuhakikisha kuwa tunatengeneza mazingira salama ya umoja na ya kumjumuisha kila mtu, ambapo washiriki wetu wa timu wanaweza kufanikiwa na kufanya kazi vizuri na wenzetu.

Kanuni yetu ya Maadili ni nyenzo ya kujenga uaminifu. Kanuni hii unaongoza vitendo na maamuzi yetu, ili kuhakikisha kwamba sote tunatendeanza kwa heshima, usawa na uadilifu, zaidi ya lawama. Kwa kweli, msimbo huu ni nyongeza ya maadili ya msingi ya TNC, na inatoa mifano wazi ya jinsi tunaweza kuishi maadili hayo kila siku. Pia hutupa mfumo wa kushikilia watu kuwajibika kwa njia bora na sawa.

Nina imani na jamii ya TNC – Nina amini kwamba tunaweza kuunda njia endelevu na siku zijazo nzuri kwa sayari yetu ya pamoja. Kutumia kanuni hii ya maadili kama mwongozo wetu, kwa pamoja tunaweza kuunda ulimwengu ambao watu na asili hustawi.

Wako Mwaminifu,



Jennifer Morris  
Mkurugenzi Mkuu



© KATIE BRYDEN/CONSERVATION INTERNATIONAL

# *Ujumbe kutoka kwa Afisa Mkuu wa Maadili, Ushirikiano na Faragha*

Tangu nijiunge na The Nature Conservancy mnamo 2019, nimevutiwa na kujitolea kwako na shauku yako ya dhamira yetu, na kujitolea kwako kuweka maadili yetu kwa vitendo ili kufanya mazingira ya kufanya kazi ya The Nature Conservancy kuwa bora kama kazi ya uhifadhi ambayo tunafanya ulimwenguni kote.

Kanuni yetu ya Maadili ni daraja kati ya maadili na sera na taratibu zetu. Kanuni yetu inapeana kila mmoja wetu nafasi ya kuchukua hatua za kiuhakiki, ili kuonyesha dhamira yetu ya kutenda kwa uadilifu katika yote tunayofanya, na kuishi maadili yetu ili tuweze kufanya athari kubwa kwa uhifadhi iwezekanavyo, bila kujali ni wapi tunakaa katika shirika, au jinsi tunavyoshirikiana na TNC.

Timu yangu na mimi tuko hapa kukusaidia kuvumbua changamoto na hali ngumu ambazo unaweza kukabiliana nazo katika kazi yetu, na kusaidia kuhakikisha kuwa tabia zetu zinalingana na maadili yetu. Unaweza Kuuliza Swali au Ripoti Suala kupitia simu yetu ya msaada, na tutakuwepo kukusaidia.

Asante kwa kujitolea kwako kwa Kanuni yetu ya Maadili. Nimefurahiya kuwa sehemu ya shirika hili zuri, na kuwa na nafasi ya kufanya kazi na kila mmoja wako, kufikia lengo letu la kulinda ardhi na maji ambayo maisha yote yanategemea, wakati pia tukikufanya The Nature Conservancy kuwa mahali pa heshima, umoja na mahali salama pa kufanya kazi.

Wako Mwaminifu,



Michelle Beistle

Afisa Mkuu wa Maadili, Ushirikiano na Faragha



© TNC

# *Watu na Mazingira Hustawi Wakati...*

## **JITOLEA KWA MAADILI YETU**

- » Uadilifu Kuliko Lawama
- » Heshima kwa Watu, Jamii na Tamaduni
- » Kujitolea kwa Kutofautiana
- » Ulinzi Mmoja
- » Matokeo Wazi, Daima



© IAN SHIVE

Maadili yetu hubaini utambuishi wetu kama shirika na jinsi tunavyojiendesha kama watu. Yanatutia moyo wa kutenda jambo jema na kutendean vizuri. Kanuni hii imeundwa ili kutoa mwongozo tukiwa tunaendesha kazi yetu ya kila siku kwa niaba ya Uhifadhi wa Mazingira (TNC) kwa mujibu Maadili Yetu. Haitoi taarifa hususan kuhusu Sera na Taratibu Kawaida za Uendeshaji (SOPs) wala sheria na kanuni ambazo tunapaswa kuzingatia; badala yake inatoa matarajio kuhusu tabia ya kimaadili ambayo yanatuhusu sote katika kazi yetu kwa ajili ya TNC. Maadili na kanuni ambazo tunapaswa kuzingatia pia huonyeshwa katika Sera za TNCs na SOPs.

## **ELEWA MATARAJIO NA MAJUKUMU YETU**

Kanuni inahusu wafanyakazi wote wa TNC kote ulimwenguni, washiriki wa bodi, wadhamini, wafadhili, na wafanyakazi wa kujitolea kwenye taratibu zote za TNC, vitengo vya biashara, na washirika. Kila mtu anayetenda kwa niaba ya TNC anapaswa kufuata Kanuni hii na vile vile sheria, kanuni, sharti, na Sera zote za TNC na SOPs. Tunatarajia pande zingine na washirika ambao tunafanya biashara nao kujiendesha kwa njia zinazolingana na Kanuni yetu. Sera na maadili yetu hulinda zaidi kuliko sheria na mila na desturi katika baadhi ya nchi. Kwa hali hizo, sisi ambao tunafanyia kazi au tunaofanya kazi pamoja na TNC tutawekwa kwenye viwango vya juu kuanzia sasa katika Kanuni hii.

***Kanuni hii inatuhusu sisi wote. Ni muhimu kwa kila mtu, na lazima tuchukuwe ukiukaji kwa uzito.***

# Kuheshimiana

WATU NA MAZINGIRA HUSTAWI WAKATI TUNA...

## JIENDESHA KWA TABIA YA KITAALAMU NA KWA HESHIMA



© JEROD FOSTER

Katika TNC, tunaelewa kwamba jinsi tunavyojiendesha kitabia huongoza mafanikio hatimaye ya misheni yetu. Tunafanya kazi yetu nzuri zaidi tukitendeanza kwa heshima. TNC haitastahamili tabia isiyo ya kitaalamu, unyanyasaji, maonevu au mateso katika mazingira yetu ya kazi-haijalishi mahali tulipo au tunachofanya kwa ajili ya shirika. Matarajio hayo pia yanahusu matukio, ziara za kijamii, kazi ya nyanjani, na shughuli zingine, kama vile mitandao ya kijamii, ambayo huenda tukawa tunajishughulisha nayo kwa niaba ya TNC.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Shughulikia kila mtu kwa mazingatio, utaalamu na heshima.
- » Angalia tabia isiyofaa na kutoa maoni yetu tunapoiona.
- » Fikiria kuhusu jinsi vitendo vyetu vinaathiri wengine na kuepuka na maongezi yanayohusu vidokezo vya kingono au vichekesho vilivyo na msingi kuhusu tulivyo tofauti, au udhanifu wenye msingi kwenye upendelevu unaohusiana na kasumba kuhusu utofauti wetu.

### Maadili katika Kitendo

Haijalishi mahali tulipo, tunachoamini au jinsi tunavyochangia kwa TNC, sote tunatunastahili kutendewa kwa wema na mazingatio. Ukosaji wa adabu, maonevu, na vitisho havina nafasi hapa.

### 🔍 Mtazamo wa Karibu

Kwa ujumla, unyanyasaji wa kingono huhusisha tabia ya kujiendesha isiyoruhusiwa. Inaweza kuwa kimwili, kwa maandishi, au maongezi, wazi au kwa kiujanja. Inaweza kuwa kitendo chochote cha aina ya ngono ambayo mtu huona kwamba inatisha, yenye chuki, au yenye kuudhi. Mifano kadhaa huhusisha:

- Vichekesho kuhusu jinsia au mwelekeo wa kijinsia.
- Vitendo au matamshi yanayotenga au kupendekeza hadhi ya cheo cha pili kwa sababu ya jinsia au mwelekeo wa jinsia.
- Kutuma au kujadili barua pepe, picha, au ujumbe usiofaa.
- Mgusano wa kimwili usioruhusiwa au vitisho vya kimwili vyenye asili ya kingono.
- Vichekesho au maongezi yanayohusu vidokezo vya ngono.
- Maombi yanayorudiarudia ya kuwa pamoja nje ya ofisi.
- Kutoa mapendeleo au nafasi katika ubadilishaji kwa ajili ya ngono.

WATU NA MAZINGIRA HUSTAWI WAKATI TUNA...

## KUJITOLEA KWA KUTOFAUTIANA, KUTENDA KWA UHAKI NA KUNUFAIKA KUTOKANA NA TOFAUTI ZETU



© TIM CALVER

Tofauti zetu husaidia uvumbuzi na huweza kutoa mazuri zaidi kutoka ndani yetu. Mafanikio yetu hutegemea uwezo wetu wa kujifunza kutoka kwa nguvu na tofauti za mtu mwingine. Tunashughulikia kila mtu kwa heshima tunapochukua wakati wa kuelewa historia na imani zao, kwa hivyo tunajua jinsi wanavyochukulia heshima.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Sisitiza utofauti katika orodha zetu za waombajikazi na majopo ya mahojiano.
- » Chukua maamuzi ya kazi kulingana na hati tumbulishi na ujuzi wa mtu, ikiwemo utofauti wa maoni na uzoefu.
- » Jumuisha watu wote na kusikiliza mawazo yao kwa heshima-hata kama yanatofautiana na yetu.
- » Tafuta kujifunza mawazo mapya kutoka kwa watu wenye uzoefu na maoni tofauti.

### Maadili Katika Kitendo

Utofauti wetu hutoa nafasi kwa ajili ya kufanya kazi pamoja kwa ufanisi zaidi. Kuchukua tofauti kama nafasi kwa kuhakikisha jumuisho ni muhimu tunapofanya kazi pamoja kama wafanyakazi wenzi. Na pia ni muhimu kazi yetu ikienda zaidi ya kuta za TNC na kwenda kwa ulimwengu unaotuzunguka kutoka kwa jamii tunayoifanyia kazi hadi kwa wafadhili na washirika ambao wanatusaidia.

### 🔍 Mtazamo wa Karibu

Maadili yetu pamoja na sheria zimeundwa ili kulinda watu wasishughulikiwe kwa njia isiyo ya haki kwa kutegemea sifa bainifu binafsi kama vile:

- Ukabila, rangi, taifa au eneo ya asili,
- Dini
- Umri au ulemavu
- Ngono, mwelekeo wa jinsia, au utambulisho wa jinsia, au
- Hali ya jeshi au aliyestaafu kwa jeshi.

## KUJISHUGHULISHA KATIKA MAZUNGUMZO BORA



© KEVIN ARNOLD

Tunapoboresha ubora wa maongezi, tunaboresha uhusiano, ubunifu, na matokeo. Tunaepuka na kujihusisha kwenye maongezi kwa nia ya kuwa sawa, kushinda, kusadikisha au kushinda maoni ya mtu mwingine. Tunajitolea kusikilizana kwa kutengeneza njia nzuri zaidi ya kwenda mbele.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Sikiliza ili kuelewa badala ya kukubali tu, kukataa au kurekebisha.
- » Onyesha heshima kwa wengine kwa kushirikisha taarifa inayofaa na muhimu.
- » Leta mawazo wazi na utayari wa kujifunza kuhusu na kutoka kwa uzoefu na maoni ya wengine, na vile vile kuonyesha uzoefu na mawazo yetu.
- » Weka mkazo kwenye mambo hakika na malengo ya pamoja ili kuboresha muungano na kukaza mwendo wa mafunzo.
- » Tambua na kuheshimu mitindo yetu tofauti ya mawasiano na njia za kuelewa kulingana na uzoefu, utambulisho, majukumu ya kishirika na historia za kitaalamu.

### Maadili Katika Kitendo

Kuunganisha kwenye kilicho muhimu kwa watu tayari, badala ya kujaribu kuwasadikisha kubadilika, ni njia moja tunaweza kukuza miungano kutoka kwa mtu kwa mwingine ambayo hujenga maadili katika TNC.

#### Mtazamo wa Karibu

Sote tuna mapendeleo ya jinsi tunavyopenda kuwasiliana. Baadhi ya hayo huweza kulingana na utamaduni. Baadhi ya watu hupendelea mawasiliano ya maandishi, na baadhi ya wengine hupendelea kwa mdomo. Baadhi hupenda kuongea kuhusu mawazo yao yanapowafikia, na baadhi hupenda kuunda mawazo yao kabla ya kuwasiliana. Baadhi wangependelea kuwa wazi wazi na moja kwa moja, na baadhi ya wengine wangependelea kutumia mawasiliano yasiyo ya moja kwa moja na kusikiliza kwa kimya. Tunapofanya kazi pamoja, tutakuwa na uzalishaji zaidi tutakapotambuwa mitindo yetu tofauti ya mawasiliano, kusaidiana kupata mambo hakika tunayoshikiana na kuongea kwa heshima.



# Kuheshimu Ulimwengu

WATU NA MAZINGIRA HUSTAWI WAKATI TUNA...

## HESHIMU JAMII ZOTE



© AMI VITALE

Kwa TNC, ushirikiano na jamii ulimwenguni hutuwezesha kutimiza misheni yetu. Tunatambua umuhimu wa msaada na maoni kutoka kwa jamii ya ndani na wenyeji katika maamuzi tunayofanya na jinsi tunavyoendelea mbele. Tunaonyesha heshima kwa watu wote na tamaduni za ndani, mahali popote tunapofanyia kazi.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Fanya kazi pamoja na wengine, kupita mipaka na tamaduni mbalimbali, ili kuelewa vizuri zaidi changamoto zinazotukabili ulimwenguni na kuendeleza masuluhisho mazuri zaidi ili kuzitatua.
- » Shirikiana na jamii za ndani ili kuhakikisha kwamba tunaheshimu daima tofauti zetu na kwamba vitendo vyetu haviundi madhara.
- » Epuka hali zinazoweza kusababisha unyonyaji wa watu dhaifu.
- » Jitahidi kuendeleza haki ya jinsia na haki kwa ajili ya watu wanyonge katika kazi yetu.

## Maadili Katika Kitendo

Tunaunda masuluhisho ya kufikiria na kushirikiana yenye athari ya muda mrefu tunapoheshimu mazoea na mila na desturi tofauti. Kujufunza kuhusu jamii za ndani hutuwezesha kuelewa vizuri zaidi jinsi ya kuonyesha heshima na uzingativu katika tamaduni.

### 🔍 Mtazamo wa Karibu

TNC hufanya kazi katika majimbo 50 ya Marekani and ulimwenguni katika nchi zaidi ya 70. Tunashawishi watu katika jamii ndogo na kubwa kupitia Ajenda ya Uhifadhi Inayoshirikishwa ambayo huweka kipaumbele kwenye miradi katika maeneo yetu muhimu ya uhifadhi. Tunaendeleza na kutekeleza miradi hii katika jamii zenye vipaumbele na mahitaji mbalimbali. Kwa kuzingatia vipaumbele na mahitaji ya jamii, tunaweza kutambua maeneo ya pamoja ambayo, yanapotatuliwa pamoja, huongoza kuelekea kazi ya uhifadhi yenye mafanikio.

WATU NA MAZINGIRA HUSTAWI WAKATI TUNA...

## KUHESHIMU KUUNGA MKONO UENDELEZAJI WA HAKI ZA KIBINADAMU



© BRIDGET BESAW

Tunaheshimu na kuunga mkono uendelezaji wa haki za kibinadamu za watu wote kupitia kwa uendeshaji wetu ulimwengu. Tunaelewa kwamba malengo na misheni zetu havipaswi kuwa muhimu zaidi ya haki za watu wanaoishi katika jamii tunazotumikia.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Heshimu haki za kila mtu na za kila mtu katika jamii zote ambapo tunatumikia.
- » Kataza kazi ya watoto, kazi ya utumwa usiolipwa na utumwa katika uendeshaji wetu.
- » Shughulikia wafanyakazi wetu kwa haki, tunawalinda kutokana na unyonyaji na matumizi mabaya katika uendeshaji wetu na kufuata sheria zinazofaa za kazi na ajira.
- » Hakikisha kuna usalama katika mahali petu pa kazi.

### Maadili Katika Kitendo

Jinsi tu tulivyo na jukumu la kuheshimu na kuendeleza haki za kibinadamu katika uendeshaji wetu ulimwenguni, pia ni lazima tukague vitendo vya wale watu wanaofanya kazi kwa niaba ya TNC ili kazi yao kwa ajili yetu ilingane na wajibu wetu wa kuheshimu haki za kibinadamu. Hatutaruhusu ukiukaji wa haki za kibinadamu kwa masingizio ya kazi yetu ya uhifadhi.

### Mtazamo wa Karibu

Ukiukaji wa haki za kibinadamu ni pamoja na kutendewa vibaya au matumizi mabaya hadi unyonyaji au utumwa wa watu au makundi. Unaweza kujumuisha matumizi ya kazi ya watoto, hali duni za kazi, kazi ya utumwa isiyolipwa, uuzaji wa watu, au matumizi mabaya na unyonyaji. Huweza pia kujumuisha hali ambapo wenyeji mahsusi na makundi mengine wanatishwa na uvamizi wa ardhi, kunyimimwa haki za kuwa na ardhi au unyakuzi, au wakati wenyeji wanaponyimwa haki ya makubaliano huru ya awali na yenye kufahamisha.

WATU NA MAZINGIRA HUSTAWI WAKATI TUNA...

## KUTENDA KWA UENDELEVVU KATIKA KAZI YETU



© CARLTON WARD JR.

Katika TNC, kuhakikisha kwamba tunaendesha kazi katika njia endelevu ya kimazingira ni sehemu muhimu ya misheni yetu ya kulinda ardhi na maji vyetu ambavyo maisha yote yanategemea. Ni pia tunavyotarajia kutoka kwetu na vile vile washirika, wafadhili, na washirika wa nje wanavyotarajia kutoka kwetu. Kuongoza kwa mfano ndivyo tunavyohamasisha wengine kutenda kwa uendelevu.

### KWA TNC, TUNA...

- » Kuanzisha malengo yenye uendelevu.
- » Kuchunguza nyayo yetu ya kaboni kwa ajili ya kuweka kipaumbele kwa juhudi endelevu zetu.
- » Kufuatilia maendeleo na kurekebisha vipaumbele vyetu kama inavyotakikana ili kufikia malengo yetu yenye uendelevu.

### Maadili Katika Kitendo

Tunajitolea kuweka malengo yanayotegemea sayansi ya kupunguza utoaji wa hewa na kushirikisha hadharani malengo yetu kuelekea kuyafikia. Tunachagua kufanya kazi na watu na mashirika wanaounga mkono kujitolea kwetu kuhusu uendelevu na mazingira.

### 🔍 Mtazamo wa Karibu

Tunaunga mkono mitindo ya usafiri isiyotoa gesi au inayotoa kiwango cha chini cha gesi na tunakuza matukio kama vile Changamoto ya Usafiri Asilia (Green Commuter Challenge) ili kuwapa wafanyakazi wetu nafasi za kuonyesha kujitolea kwetu kuhusu uendelevu katika uendeshaji wetu. Tunathamini kwamba mafikio yetu ulimwenguni yana matokeo muhimu ya usafiri wa ndege, yenye madhara kwenye mazingira. Tutafanyakazi ili kupunguza athari ya safari za biashara kupitia hatua za kukabiliana zinazofaa, zikijumuisha, kwa mfano, matumizi ya maongezi ya mbali yanayotumia video. Tunajitahidi kupunguza nyayo ya kaboni kwa kutumia vyanzo vya nishati mbadala na kufanyia kazi katika majengo yenye nishati fanisi. Tunaunga pia mkono mazingira kupitia uchafu endelevu na mazoea ya uozeshaji-mbolea katika mengi ya majengo yetu.

# Kutenda kwa Uadilifu

WATU NA MAZINGIRA HUSTAWI WAKATI TUNA...

## FUATA SHERIA NA MASHARTI YANAYOFAA NA KUEPUKA NA ULAGHAI, WIZI NA UFISADI



© JEFF YONOVER

Tunafuata sheria na masharti yanayofaa na kuhakikisha Uadilifu Badala ya Lawama. Hatutoi au kukubali rushwa kwa kubadilishana na vitendo vya kupendelewa, haijalishi mahali tulipo au yule tunayefanya naye kazi. Tunafuata sheria zote ulimwenguni ambazo zinazotawala rushwa na ufasidi. Tunatekeleza sera, taratibu na udhibiti ili kutusaidia kugundua na kuzuia utakatishaji wa pesa haramu na utoaji wa pesa za kusaidia vitendo vya kigaidi.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Kamwe hatutoi au kukubali kitu cha thamani ili kushawishi visivyostahili uamuzi au utendeaji kwa ajili ya kupendelea TNC.
- » Toa usimamizi wa kazi ya wawakilishi ambao wanatenda kwa niaba ya TNC ili kuhakikisha kwamba vitendo vyao vinalingana na maadili na viwango vyetu.
- » Jua kwamba sheria ambazo zinakataza rushwa na ufasidi pia hutumiwa kwa pesa zinazotolewa na serikali na michango, kukiwemo michango ya kutoa misaada.
- » Elewa kwamba sheria maalum hufaa wakati sisi, au wawakilishi wetu wanafanya kazi pamoja na maafisa wa serikali.
- » Tenda kwa uangalifu na tahadhari kama kazi yetu inashughulisha uendeshaji ambao upo katika hatari ya hali ya juu ya utakasaji wa pesa haramu na utoaji wa pesa kwa wagaidi.

### Maadili Katika Kitendo

Kutoa zawadi, burudani au malazi katika harakati za kuendesha biashara huweza kuwa mazoea na kisheria katika pande fulani za ulimwengu. Lakini kubadilishana vitu vya thamani kawaida huweza kuonekana kama rushwa. Na rushwa siyo lazima ishughulishwe daima pesa, inaweza kuwa kufanyia upande mwingine upendeleo kama vile huajiri mtu wa familia ili kufanyia TNC. Tukitoe au kupokea zawadi au kulipa safari au malazi mengine, hasa kwa maafisa wa serikali, tunahakikisha kuwa kufanya hivyo kunafaa na hakuna nia ya kushawishi maamuzi ya biashara visivyo vya haki au kununua upendeleo.

### 🔍 Mtazamo wa Karibu

Kuna sheria zaidi kali zinazofaa wakati tunafanya kazi na maafisa wa serikali, wakiwemo watu wanaofanyia kazi makampuni yanayomilikiwa na serikali kwa kiasi fulani tu au kikamilifu. TNC inaweza kuwajibikia vitendo vya wakilishi, wakiwemo washauri huru, mawakala na wanakandarasi ambao hufanya kazi kwa niaba yetu. Ukijihusuisha na wawakilishi kwa niaba ya TNC, hakikisha kwamba unajua yule ambaye unafanya kazi naye na kwamba vitendo vyao vinalingana na sera zetu, Kanuni hii na sheria. Baadhi ya maonyo ya kuangalia yanajumuisha wakati Afisa wa Serikali au Mshirika:

- Anapendekeza mtu au kampuni maalum kugawa bidhaa, kusaidia kupata rufusa, au kutoa baadhi ya huduma nyengine.
- Anaomba malipo, kama vile mchango wa pesa, yafanywe moja kwa moja kwa mtu.
- Anaomba ada ambayo ni kubwa zaidi kuliko kiwango cha soko kwa kazi inayolingana bila maelezo yanayoeleweka.
- Anaomba malipo katika taslimu.
- Hawezi au hatatoa marejeo yanayoaminika.

WATU NA MAZINGIRA HUSTAWI WAKATI TUNA...

## WANATENDA KAMA WASIMAMIZI WAZURI WA PESA ZOTE ZA MCHANGO NA MFADHILI



© MAC STONE

Tunatumia fedha za hadhira au binafsi, katika muundo wowote, ili kuendeleza misheni ya TNC tu. Wakati wafadhili wetu wanapochangia TNC, wanatuamini kutumia michango yao kwa ufanisi na rasilimali zilizopo katika njia inayoendeleza mbele malengo yetu tunayoshirikiana kwa ajili ya shirika.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Tenda kwa uwajibikaji kwa gharama za biashara yetu na tunakumbuka kujitolea kwetu kwa kusimamia rasilimali ya wafadhili wetu na TNC kwa kufikiria katika matumizi yetu ya pesa.
- » Tuma marudishio ya pesa zilizotumiwa tu kwa ajili ya gharama za biashara zinazokubaliwa kama inavyoelezwa katika SOP yetu and kamwe si kwa matumizi binafsi ya pesa.
- » Weka kumbukumbu kwa makini jinsi tunavyotumia pesa na kufuata mahitaji ya uhasibu na kisheria ambayo yanalingana na mapokezi na matumizi ya pesa.
- » Toa ahadi kwa wafadhili tu ikiwa tunajua kwamba tunaweza kuziheshimu na kutumia pesa za wafadhili kulingana na nia ya mfadhili.
- » Tafuta mwongozo kutoka wa Idara ya Fedha tukiwa na maswali kuhusu jinsi tunapaswa kutumia au kuweka kumbukumbu ya zawadi au mchango wa pesa.

### Maadili Katika Kitendo

Ni wajibu wetu kama shirika la utoaji wa msaada kuhakikisha tunaheshimu matumizi ya fedha za mfadhili zilizopangwa. Hili ni chaguo la kiadili na majukumu ya kuheshimu uaminifu wa wafadhili wetu. Vile vile, umaalumu wa fedha tunazopewa kupitia pesa za michango zinapaswa kufutiliwa daima.

### 🔍 Mtazamo wa Karibu

Nia ya mfadhili wakati mwingine huonyeswa wazi na mfadhili; wakati mwingine ni maandishi kwenye hundi binafsi, au barua inayoletwa pamoja na mchango. Haijalishi jinsi mfadhili atachagua kuwasiliana, tunaweka kumbukumbu hizi ili kufikiria kuhusu nia ya mfadhili wakati mchango unapokewa na uhamisho wote au matumizi ya fedha halafu tunafuata nia ya mfadhili.

WATU NA MAZINGIRA HUSTAWI WAKATI TUNA...

## KAA SALAMA NA ULINDE WENGINE



© CARLTON WARD JR.

Kutokana na asili ya kipekee ya kazi yetu katika TNC, tuna wajibu wa kukaa salama na kulinda usalama wa wengine katika shughuli zetu pana kote ulimwenguni. Hii inajumuisha kuhakikisha kwamba mahali pa kazi yetu panabaki bila ukatili, kama vile kutokana na matumizi ya madawa ya kulevya na pombe. Ni muhimu pia kuchukua tahadhari zinazofaa wakati tunapofanya kazi kwenye uhifadhi wetu, pamoja au kando ya vijana, na mahali mbali vijijini na kwenye hatari.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Jua na kufuata sheria za usalama na tahadhari zinazolingana na kazi tunayofanya.
- » Kamwe haturuhusu maamuzi na uwezo wetu kuathiriwa na madawa ya kulevya na pombe wakati tunapofanya kazi.
- » Wasiliana tukihisi hatuna usalama au tuna wasiwasi kwamba mtu fulani huenda akawa hana usalama.
- » Tambua kuwa kazi katika mahali mbali vijijini au kwenye hatari au kwenye uhifadhi huweza kusababisha hatari ya usalama ya kipekee na kuchukua hatua zinazofaa ili kuzuia madhara.
- » Elewa na kufuata taratibu zote za usalama, kukiwemo zile za safari, gari, udhibiti wa moto, mashua, mbizi, bunduki na vijana.

### Maadili Katika Kitendo

Tunachukua usalama kwa uzito sana na kufuata sheria na mahitaji yote ya usalama ambayo yanalingana na vitu vyote tunavyofanya-kuanzia kufanyia kazi ndani ya ofisi hadi kuendesha gari la TNC. Tukiwa tunapiga mbizi, kuendesha mashua, kuendesha fueli uliyoandikiwa au kufanya kazi ya nyanjani, tunachukua tahadhari zaidi tunapokuwa tunafanya kazi mahali mbali vijijini ambapo ni vigumu zaidi kupata usaidizi wa haraka majeruhi yanapotokea.

### Mtazamo wa Karibu

Kazi yetu ya uhifadhi mara nyingi hutupeleka katika mahali mbali vijijini na kwenye hatari. Ili kuepukana na majeruhi makali au vibaya zaidi, ni muhimu kupanga na kujitayarisha kwa ajili ya uwezekano wa usalama na hatari za kimatibabu. Tunatoa rasilimali za ndani na za nje ili kusaidia wafanyakazi na washiriki wetu kubaki salama wakati wa kufanya kazi ya TNC.

## KUEPUKA NA MIGONGANO YA MASLAHI



© KEVIN ARNOLD

Migongano ya Maslahi hutokea wakati mtu aliye na wajibu wa kutenda kwa maslahi mazuri zaidi ya TNC ana maslahi mengine yanayoweza kushawishi au kuathiri, au kuonekana kushawishi au kuathiri, uwezo wa mtu kutenda kwa maslahi mazuri zaidi ya TNC. Katika TNC, tunaepuka na migongano ya maslahi na mwonekano wa migongano ya maslahi.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Elewa maana ya kuwa na migongano ya maslahi.
- » Wasiliana na (Idara ya) Maadili na Sheria ikiwa tunafikiri tunaweza kuwa na migongano ya maslahi au tunashughulika katika kitendo kichoweza kuonekana kama mgongano wa maslahi.
- » Shughulikia migongano vizuri ili tuwe na haki katika shughuli zetu zote.

### Maadili Katika Kitendo

Wadau wetu, kukiwemo wafadhili wetu, huwekeza kwetu kwa sababu wanatutegemea ili kuweka mbele misheni ya TNC. Kuepuka na migongano ya maslahi hutuwezeshwa kuendeleza sifa zetu kama sababu inayostahili mchango.

### 🔍 Mtazamo wa Karibu


Hii hapa ni mifano ya hali ambapo migongano huweza kutokea:

- Kujihusisha na ajira ya mtu wa familia au rafiki wa karibu.
- Huduma kwenye bodi ya shirika ambayo ina au huweza kuwa na shughuli na TNC, inahusiana na TNC au huweza kufanya vitendo vinavyoathiri TNC.
- Kujihusisha na ajira ya nje au kazi ya kujitegemea ambayo inayoingilia uwezo wako wa kufanyia kazi TNC.
- Kuendeleza uhusiano wa kuripoti ambao unaathiri uwezo wako wa kuwa yakinifu (kama vile kuwa na uhusiano ambapo mtu wa familia anaripoti kwako).
- Kugombea Uchaguzi wa Ofisi ya Umma.
- Kukubali zawadi au burudani ambayo inaweza kuathiri jinsi unavyofanya maamuzi.

# Kulinda TNC

WATU NA MAZINGIRA HUSTAWI WAKATI TUNA...

## JITAHADHARI KWA MITANDAO YA KIJAMII NA KAULI ZA HADHARANI KUHUSU TNC



© ALEX SNYDER/TNC

Katika TNC, jinsi tunavyowasiliana kuhusu shirika hunaweza kuwa na athari muhimu kwa sifa zetu ulimwenguni. Ni muhimu kuongea wazi, kikamilifu na kwa uangavu kuhusu TNC na kuheshimu wajibu wetu kama wafanyakazi ili kulinda taarifa ya siri.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Tenda kwa utaalumu, kwa adabu na kwa heshima katika mawasiliano yanayohusu kazi.
- » Toa taarifa rasmi kwa vyombo vya habari au kwa watu kwa ajili ya TNC kwa ruhusa inayofaa tu kufanya hivyo.
- » Epuka kushirikisha taarifa ya siri kuhusu TNC na uonyeshe tahadhari ile ile kwa taarifa ya siri ya wengine.
- » Fanya wazi kwamba imani zetu ni imani zetu wenyewe na siyo imani za TNC, isipokuwa mawasiliano yetu yanafanywa kwa niaba yetu na yameruhusiwa na TNC.

### Maadili Katika Kitendo

Tunapotumia tovuti za mitandao ya kijamii kwa kuwasiliana na kushirikisha mawazo yetu, watu wengi ulimwenguni huweza kupata ufikivu wa tovuti. Kwa kuchagua maneno yetu kwa makini, tunajitambua wenyewe na TNC kwa heshima.

### 🔍 Mtazamo wa Karibu

Mitandao ya kijamii huhusu tovuti na programu ambapo watu wanashirikisha na kujishirikisha katika mitandao ya kijamii. Kwa mfano, mitandao ya kijamii hujumuisha tovuti kama vile Instagram, Facebook, Snapchat, Twitter, Weibo, WeChat, WhatsApp, YouTube, na kadhalika. Mitandao ya Kijamii huweza kuwa jukwaa yenye ufanisi wakati tunaitumia kwa wajibu katika kazi yetu kwa ajili ya TNC ili kukuza na kushirikisha mawazo yetu na kuwasiliana na waasiliani na marafiki.



## HIFADHI HALI YETU YA UTOAJI WA MISAADA



© IAN SHIVE

Kama shirika la utoaji wa misaada kwa watu, TNC hupata baadhi ya maslahi, na vile vile majukumu muhimu. Kuendeleza Kiwango cha TNC, kazi yetu inapaswa kuendeleza misheni yetu. Tunachukuwa majukumu yetu kwa uzito na kufuata viwango hivi mahali popote tunapofanya kazi ulimwenguni. Hii hujumuisha majukumu ambayo yanahusiana na mazoea ya uhasibu, na vile vile kushawishi na vitendo vya kisiasa.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Fuata sheria na kanuni za kushawishi ambazo zinalingana na kazi tunayofanya kwa ajili ya TNC na kuepuka na kushawishi vinavyopita kiwango.
- » Fuatilia wakati wote na kuhusiana na rasilimali za kushawishi zinazofuata Sera na Taratibu zetu.
- » Epuka na kuunga mkono au kupinga chama au mgombea wa kisiasa anayegombea ofisi ya umma wakati tunawakilisha TNC, kukiwemo matukio ya hadharani na kwenye mitandao ya kijamii.
- » Endeleva kumbukumbu sahihi za kifedha kwa ajili ya malengo ya ukaguzi na uhasibu na kutuma ushuru wote unaohitajika na ripoti za kampuni.

### Maadili Katika Kitendo

Sifa yetu kama shirika la mchango lenye heshima ya hali ya juu hutuwezesha kuendelea kufanya kazi tunayofanya. Sisi wote tuna wajibu wa kulinda sifa yetu kwenye kila zamu. Kuanzia kwa kuepuka migongano ya maslahi hadi kuonyesha uangavu katika mambo yote tunayofanya, hadi kufuata sheria zote zinazotufaa-wafadhili wetu na wetu wengine wanatutegemea daima kufanya jambo la haki.

### Mtazamo wa Karibu

Ingawa hatuwezi kuunga mkono au kupinga chama au mgombea wa kisiasa katika uwezo wetu wa TNC, tunaweza kufanya hivyo kama watu binafsi. Hii ina maana kutotumia rasilimali yoyote ya TNC (kama vile barua pepe, nafasi ya ofisi, au wakati) au kuvaa nguo zenye alama ya TNC ili kuunga mkono mgombea yeyote. Kama kutuma mambo ya kisiasa kwenye mitandao ya kijamii, watu wanaweza kujumuisha makanusho kwenye ukurasa wao binafsi kwamba wanafanya hivyo kwa uwezo wao binafsi na siyo kama mwakilishi wa TNC. Ni muhimu kutoongoza mtu yeyote kuamini kuwa tunaongea kwa niaba ya TNC katika mukhtadha wa kisiasa.

## WEKA TAARIFA YA SIRI SALAMA NA KUESHIMU FARAGH



© CARLTON WARD JR.

Katika mwendo wa kazi yetu kwa ajili ya TNC, tunafikia taarifa ya siri, ikiwemo data binafsi ya wafanyakazi, wafadhili na washirika. Ni wajibu wetu kuheshimu usiri wa mtu mwenye data binafsi tunayokusanya au kuwa na ufikivu kwa kuweka kikomo kwenye kiasi cha data tunayokusanya na kwa kuilinda. Tunafuata sheria ambazo hulingana na ukusanyaji, uwekaji, na matumizi ya data binafsi kila mahali tunapofanya biashara. Zaidi ya hayo, tunapaswa kuweka taarifa zote za siri kuhusu kazi yetu kwa ajili ya TNC kwa usalama kila wakati.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Shirikisha taarifa binafsi ndani au nje ya shirika na wale wanaohitaji kujua tu na wanaohidi kulinda taarifa hiyo.
- » Tumia taarifa ya siri tu wakati wa kazi yetu kwa niaba ya TNC -na siyo kwa sababu binafsi.
- » Kamwe usijadili au kushirikisha taarifa ya siri tunayotambua katika kazi yetu kwa ajili ya TNC na mtu mwingine nje ya TNC au mtu yeyote ndani ya TNC ambaye haimhusu kuijadili.

### Maadili Katika Kitendo

Kazini, tunapaswa daima kufikiria kuhusu kuweka taarifa ya siri kwa usalama. Kwa mfano, wakati wa kujadili taarifa ya siri, hakikisha kwamba upo katika nafasi binafsi ambapo wengine hawawezi kukusikia. Na uweke kompyuta yako ya kupakata na vifaa vingine vinavyobebeka katika mahali salama na ufunge vikiwa havitumiwi.

### 🔍 Mtazamo wa Karibu

Taarifa ya Siri inaweza kujumuisha:

- Taarifa kuhusu wafadhili wetu na washirika,
- Taarifa kuhusu wafanyakazi wetu,
- Miradi kwenye upeo, au
- Majadiliano na watu wanaoweza kuwa washirika wapa.

WATU NA MAZINGIRA HUSTAWI WAKATI TUNA...

## LINDA MALI YA KITAALUMA



© NICK HALL

Mali yetu ya kitaaluma husaidia chapa yetu na kufafanua utambulisho wetu kama shirika. Kuelewa jinsi ya kuitambua hutuwezesha kuilinda kwa wakati wote.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Jua jinsi ya kutambua mali ya kitaaluma na kuilinda kila siku.
- » Hakikisha kwamba tuna haki ya kutumia mali ya kitaaluma ya wengine kabla hawajaitumia.
- » Uliza maswali au tafuta mwongozo tukiwa na wasiwasi kuhusu hali ya kama kitu ni mali ya kitaaluma na kama tunahitaji kuchukua hatua za kukilinda.

## Maadili Katika Kitendo

Jina na nembo ya TNC ni alama na ni zenye thamani, mali inayolindwa. Tunaweza tu kuruhusu wengine kutumia jina na nembo yetu wakiwa sambamba na misheni, na matumizi yameidhinishwa. Wakati tunaposhirikiana na wengine katika uhusiano wa masoko, tunapaswa kuhakikisha ushirikiano huo umerudiwa na kuidhinishwa ili kulinda chapa yetu. Tunaheshimu pia mali ya kitaaluma ya wengine na tunatumia picha, muziki, na chapa ya wengine tu kwa idhini yao.

### Mtazamo wa Karibu

Baadhi ya mifano ya mali ya kitaaluma ya TNC inajumuisha:

- Alama, kama vile jina na nembo ya TNC,
- Hakimiliki, kama vile kifaa kinachoeleza data ya kisayansi, kukiwemo vitabu,
- Siri za biashara ya ubadilishaji, au
- Umilikaji.

WATU NA MAZINGIRA HUSTAWI WAKATI TUNA...

## KULINDA RASILIMALI ZA TNC NA KUTUMIA MIFUMO YA TAARIFA KWA WAJIBU



© AMI VITALE

Kulinda rasilimali za TNC na kuzilinda kuibiwa, kutupwa, au kuathiriwa ni wajibu muhimu sana wa sisi wote. Kama wasimamizi wa TNC, tunalinda rasilimali zetu zenyewe na vile vile rasilimaliza kifedha na mifumo ya teknolojia na taarifa.

### KATIKA TNC, TUNA...

- » Weka kwa tahadhari mali yote inayomilikiwa na TNC-kuanzia kwa magari yanayomilikiwa na shirika hadi nafasi ya ofisi na vifaa vinavyotumiwa katika utafiti na uendeshaji wa biashara.
- » Onyesha uamuzi mzuri wakati wowote unapotumia mifumo ya taarifa na teknolojia ya TNC.
- » Tumia mifumo ya taarifa na teknolojia kwanza kwa ajili ya malengo ya kibiashara na kuweka kikomo kwa matumizi binafsi kwa chini ya asilimia 10 ya matumizi yote.

### Maadili Katika Kitendo

- Jinsi tunavyotumia rasilimali yetu husema mengi kuhusu wale tulio kama shirika. Katika TNC, sisi hutumia rasilimali kwa busara. Tunaposhughulikia vinavyomilikiwa na TNC kwa tahadhari ile ile tunavyotumia kushughulikia mali yetu wenyewe binafsi, tunakuza utamaduni wa heshima.

### Mtazamo wa Karibu

Kuna vitendo ambavyo tunaweza sisi wote kuchukua ili kulinda uadilifu wa mifumo yetu ya taarifa na teknolojia-kuanzia jinsi tunavyowasiliana hadi tunavyoweke taarifa kwa usalama. Kwa mfano:

- Tambua na kuripoti barua pepe unazoshuku kwenye mtandao wetu zinazoweza kuwa na nia ya kutuiba au kutusababishia madhara.
- Epuka na kutembelea tovuti au kupakua programu zisizoidhishwa na TNC.
- Tumia maneno ya siri yenye nguvu.
- Fuata maelekezo kutoka kwa IT (Teknolojia ya Taarifa) ili kulinda mifumo na data zetu.

# Kujitolea Kwetu

Katika TNC, watu na mazingira hustawi tunapofuata Kanuni hii na kutafuta mwongozo tunapokuwa na maswali.

Sisi wote tuna wajibu wa kutoa maoni ikiwa kuna kitu kisichoendelea vizuri au ikiwa tuna mashaka kuhusu mwenendo mbaya kimaadili, ikiwemo tukiona tabia isiyofaa au ukiukaji of Sera na SOPs zetu.



© SAM LAWRENCE/TNC PHOTO CONTEST 2019

## **NINI ITAFANYIKA NIKIFANYA RIPOTI?**

Kuna watu wengi katika TNC kwa ajili ya wafanyakazi na pande zingine wa kufikia ukiwa unataka kuuliza swali au unahitaji kuripoti wasiwasi kuhusu mwenendo mbaya or uwezekano wa mwenendo mbaya. Kama wewe ni mfanyakazi, unaweza kuwasiliana na msimamizi wako, mwangalizi mwingine wa TNC, mshirika wa kikundi cha Maadili na Sheria au mshirika wa Kikundi chetu cha Umma.

Wafanyakazi na pande zingine wanaweza kuwasiliana na kikundi cha Maadili na Sheria wakati wowote ili kutuma swali au shaka kwenye mstari wetu wa msaada mtandaoni, [www.nature.or/tnc Helpline](http://www.nature.or/tnc Helpline). Lainii ya TNC wa Msaada unapatikana mtandaoni au kwa simu saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki katika mbalimbali. Maswali na mashaka huweza kutumwa kisiri bila kujitambua. Ukipiga laini yaa msaada, utaongea na afisi wa upande mwingine ambaye ataandika shaka na kutuma kisiri kwa kikundi cha Maadili na Sheria. Ukituma swali au shaka mtandaoni, litafika moja kwa moja kwa Kikundi cha Maadili na Sheria.

## **NINI ITATOKEA KAMA MTU ANALIPIZA KISASI DHIDI YA MFANYAKAZI KWA SABABU AMETOA RIPOTI?**

TNC haitaruhusu ulipizaji wa kisasi dhidi ya watu watakaouliza maswali au kuonyesha wasiwasi kuhusu uwezekano wa mwenendo mbaya kwa nia nzuri. Tunatarajia kila mmoja katika TNC kutoa maoni ikiwa wanaamini kwamba mtu au kundi la watu wanaokabiliwa na ulipizaji wa kisasi.

Ulipizaji wa kisasi hutokea kwa aina nyingi tofauti na huweza kutokea kwa uwazi au kwa uficho. Unaweza kutokea ukianzia kwa udhalilishaji wa maneno na vitisho - kukiwemo kuchukua vitendo hatari vya kikazi kama vile kushusha mtu cheo au kukatisha mtu kutaka kupandishwa cheo - kwa aina nyingine zinazofichama kama vile kutoalika mtu kwa starehe ya kundi, kuongea vibaya kuhusu mtu kwa wafanyakazi wengine, kwa kutoa nafasi kidogo za maendeleo binafsi au kumfanyisha mtu kazi kwa cheo cha chini ambaye ana uwezo wa michango zaidi muhimu. Tukipata ushahidi wa ulipizaji wa kisasi, tutatia nidhamu mwenye kulipiza kisasi, hadi na kukiwemo hata kufutwa kazi.

**Ni swala la ujasiri mkubwa kutoa maoni. Tunaonyesha kujitolea kwetu kwa Maadili Yetu kwa kuungana mkono wakati wasiwasi na matatizo yanapotokea.**